

YOSEFU

KADI YA
BIBLIA
11

MASWALI

- A.** Jaza mapengo. Ndugu wa kambo wa Yosefu walimwita “yule _____,” na wakamwaza utumwani kwa vipande _ vya fedha.
- B.** Aliposhinikizwa na mke wa Potifa wafanye ngono, Yosefu alijibu hivi kwa ujasiri, “Ninawezaje kufanya ubaya huu mkubwa na . . .”
- C.** Kwa nini Farao alimweka Yosefu kuwa mtawala wa pili wa Misri?



4026 K.W.K.

Adamu
aumba

Alilishi katika miaka
ya 1700 K.W.K.

1 W.K.

98 W.K.

Kitabu cha mwisho
cha Biblia kinaandikwa



YOSEFU

MAMBO MACHACHE KUMHUSU Mwana wa kwanza wa Yakobo na Raheli. (Mwanzo 35:24) Ndugu zake wa kambo wenye wivu walimwaza utumwani Misri ambako alikaa kwa miaka 13 hivi akiwa mtumwa na mfungwa. Badala ya kulipiza kisasi, Yosefu aliwasamehe ndugu zake wa kambo waliotubu. (Mwanzo 50:15-21) Ingawa alikuwa mbali na nyumbani, alimheshimu Yehova, akadumisha usafi wa maadili, akafanya kazi kwa bidii, na alikuwa mwenye kuaminika.—Mwanzo 39:1-23.

MAJIBU

- A.** Mwota-ndoto, 20.—Mwanzo 37:19, 28.
- B.** “. . . kwa kweli nimtendee Mungu dhambi?”—Mwanzo 39:9.
- C.** Alijua kwamba roho ya Mungu ilimfanya Yosefu kuwa mwenye hekima na busara.—Mwanzo 41:38-41.